Swahili

# Huduma Zingine







ipc Health

## Kuhusu sisi

# IPC Health inatoa matunzo eneo la magharibi mwa Melbourne.

Mtu yeyote anayeishi, kufanya kazi au kusoma katika maeneo ya halmashauri ya jiji la Brimbank, Wyndham au Hobsons Bay anaweza kupata huduma nyingi za afya ya jumuiya chini ya huduma  moja.

## Je, Afya ya jumuiya ni nini?

Mashirika ya afya ya jumuiya yanalenga kuboresha afya na ustawi wa jumuiya za eneo.

Yanalenga pia kuwaelimisha wenyeji kuhusu kuzuia magonjwa.

IPC Health inathamini uanuwai na imejitolea kubuni huduma salama, zinazosaidia na zinazoweza kufikiwa na watu mbalimbali, ikijumuisha, lakini sio tu:

- Wazawa na wakazi asilia wa Visiwa vya Torres Strait
- wasagaji, mashoga, watu wa jinsia mbili, watu waliobadilisha jinsia, watu wasiojitambulisha na uwili wa jinsia, watu wenye sifa za jinsia zote mbili na wasiovutiwa kingono na jinsia yoyote (LGBTQIA+)
- watu walio na ulemavu wowote
- watu walio na changamoto ya kupata huduma bora za afya mahali pengine
- watu walio na utamaduni au lugha tofauti



# Waaustralia Wazee

Huduma ya Serikali ya Australia ya My Aged Care (Utunzaji wa Wazee) inawawezesha Waaustralia wazee (wenye umri wa miaka 65 na zaidi, na Wazawa na wakazi asili wa Visiwa vya Torres Strait wenye umri wa miaka 50 na zaidi) kupata huduma na mipango ya utunzaji wa wazee.

Ikiwa ungependa kupata usaidizi ukiwa nyumbani, unaweza kutuma ombi kupitia My Aged Care kwa Kifurushi cha Huduma ya Nyumbani.

Kifurushi hiki hukupa udhibiti zaidi wa huduma unazopokea nyumbani.

Unaweza pia kuratibu huduma kama vile tiba ya mwili, matibabu ya miguu, tiba ya utendakazi, lishe na matibabu ya matamshi kupitia My Aged Care.

IPC Health ni mtoa huduma aliyesajiliwa na My Aged Care, kwa hivyo unaweza kuomba IPC Health iwe mtoa huduma wako unayependelea.

Kwa maelezo zaidi, tembelea myagedcare.gov.au au upige simu kwa 1800 200 422.

Wateja wazee wanaweza kuwasiliana na IPC Health moja kwa moja ili kupata huduma za afya.



# Huduma zetu

## Usaidizi wa utunzaji wa wazee na watu walio na ulemavu

- Huduma za Utunzaji wa Nyumbani
- Mpango wa usaidizi wa nyumbani
- Huduma ya IPC Health ya Kutafuta Utunzaji
- Kazi za kijamii na usaidizi wa kujitegemea



## Watoto, vijana na familia

- Kituo cha Afya na Ustawi wa Watoto cha Brimbank Melton
- Kituo cha Huduma kwa Watoto na Familia katika Wyndham Vale
- Huduma za Usaidizi wa Uingiliaji Kati kwa Familia
- Huduma ya Wyndham ya kusaidia familia za watoto waliokataa shule
- Huduma za familia
- Huduma za Kuhakikisha Afya ya Mama, na Mtoto
- Kikundi cha Usaidizi cha Hungry Caterpillars (kinachowaleta pamoja wazazi, watoto, watunzaji na washauri)
- Tiba ya utendakazi kwa watoto
- Huduma za kisaikolojia kwa watoto
- Tiba ya matamshi kwa watoto
- Mpango wa Young Leaders of the West
- Afya ya Vijana

## Matibabu na afya

- **Afya ya Wazawa na Wakazi Asili wa Visiwa vya Torres Strait**
- **Matibabu ya masikio**
- **Kuzuia saratani**
- **Mpango wa kuboresha afya ya moyo wale waliougua ugonjwa wa moyo**
- **Uuguzi wa afya ya jumuiya**
- **Huduma za matibabu ya meno**
- **Elimu ya kisukari**
- **Lishe**
- **Fiziolojia ya mazoezi**
- **Kliniki ya GP**
- **Usaidizi kwa watu wasio na makazi**
- **Mpango wa utoaji wa sindano na sirinji**
- **Tiba ya utendakazi**
- **Huduma ya matibabu ya watoto**
- **Tiba maungo**
- **Matibabu ya miguu**
- **Afya ya wakimbizi**
- **Tiba ya matamshi**
- **Afya ya wanawake**

## Afya ya akili na ustawi

- Ushauri wa kuacha kutumia pombe na dawa za kulevya
- Ushauri wa afya ya jumuiya
- Usaidizi wa kukabiliana na unyanyasaji wa nyumbani
- Usaidizi wa Kukabiliana na Uraibu wa Uchezaji Kamari
- Afya ya Akili (Head to Health)
- Usaidizi kwa Wanaume ambao Wamenyanyaswa Kingono (Living Well)
- Power Over Pain (Usaidizi wa Kukabiliana na Maumivu)

Tafadhali kumbuka kuwa huduma zingine hutolewa katika eneo moja tu.

Wengine hutoa ziara za nyumbani na/au matibabu kwa njia ya simu.

Ili kupata maelezo zaidi, piga simu kwa kituo kilicho karibu nawe au utembelee tovuti yetu kwa **ipchealth.com.au**



# Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

## Je, kuna ada inayotozwa?

Huduma zetu nyingi ni za bila malipo, hata hivyo baadhi zinaweza kutozwa ada. Tafadhali muulize mfanyakazi wako wa usajili. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kulipa, tafadhali zungumza na timu yetu ya Huduma kwa Wateja.

## Je, ninawezaje kuweka miadi?

Piga simu kwenye mojawapo wa vituo vyetu ili uweke miadi.

Huenda ukahitajika kusubiri kabla ya kupata miadi.

Unaweza kuweka miadi ya ziara kwa daktari wako mtandaoni kupitia tovuti yetu ya **ipchealth.com.au/appointments**

## Je, ninajisajili vipi kwa huduma?

Mfanyakazi wa usajili atatathmini huduma muhimu kwako na kukujulisha kuhusu maelezo mahususi kama vile gharama na nyakati za kusubiri.

## Je, ninaweza kutoa maoni?

Ndiyo.Tafadhali tembelea tovuti yetu ya ipchealth.com.au au upige simu kwa kituo kilicho karibu nawe.

## Je, ninaweza kupata mkalimani?

Ndiyo, huduma za ukalimani zinapatikana bila malipo. Tunao pia wakalimani wa Auslan (Lugha ya Ishara ya Australia). Tafadhali tujulishe unapoweka miadi.

## Rufaa na usajili

**Simu ya Jiji la Brimbank:**
1300 472 432

**Simu ya Jiji la Hobsons Bay :**
1300 472 432

**Simu ya Jiji la Wyndham:**
1300 472 432

**Simu ya Ushauri wa kuacha pombe na dawa zingine za kulevya:**
9296 1228 or 1800 700 514

**Simu ya Ushauri wa Kifedha na Usaidizi wa Kukabiliana na Uraibu wa Uchezaji Kamari:**
1400 472 432

**Simu ya Huduma za Familia za Brimbank Melton Orange Door:**
1800 271 046

**Simu ya Western Melbourne Orange Door:**
1800 271 045

## Ofisi Kuu ya IPC Health

106 Station Road
Deer Park VIC 3023
PO Box 171 Deer Park VIC 3023

**ACN** 136 685 151
**ABN** 68 846 923 225

### Deer Park

106 Station Road
Deer Park 3023

### St Albans

1 Andrea Street
St Albans 3021

### Sunshine

Level 1, 499 Ballarat Road
Sunshine 3020

### Altona Meadows

330 Queen Street
Altona Meadows 3028

### Hoppers Crossing

117–129 Warringa Crescent
Hoppers Crossing 3029

### Wyndham Vale

510 Ballan Road
Wyndham Vale 3024

**1300 472 432**

**W** ipchealth.com.au
**E** ipchealth@ipchealth.com.au

IPC Health   IPC Health   IPCHealth_au